


# Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 03 Issue: 01 | March-2024

EAJK


# Teknolojia ibuka na ufundishaji wa somo la Kiswahili


**Author**

**Anyonje M. Florence[1]; Milton Kigaro Lihanda[2]**

**Email: anyonjeflorence@gmail.com**

**(1) Chuo kishirikishi cha Bomet, Kenya; (2) Chuo kikuu cha Moi, Kenya.**



**Cite this article in APA**

Anyonje, M. F., & Lihanda, M. K. (2024). Teknolojia ibuka na ufundishaji wa somo la Kiswahili. *East Africa journal of Kiswahili*, *3*(1), 25-32. https://doi.org/10.51317/eajk.v3i1.487

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 29.12.2023
Accepted: 31.01.2024
Published: 13.03.2024

Scan this QR to read the paper online



**Copyright**: ©2024 by the author(s). This article is an open access article distributed under the license of the Creative Commons Attribution (CC BY) and their terms and conditions.



**Ikisiri**

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuchanganua teknolojia ibuka na ufundishaji wa somo la Kiswahili. Katika sekta mbalimbali kama vile afya, benki, biashara, usafiri, utawala, kilimo, ufundi na hata mawasiliano teknolojia za kisasa zinatumiwa. Sekta ya elimu haijaachwa nyuma katika matumizi ya teknolojia hizi. Utafiti huu ulizingatia nadharia ya Piaget inayosema kuwa akili ya mtoto hukua kulingana na mtagusano wake na mazingira. Matokeo ya utafiti huu ni kuwa, Teknolojia ibuka kama vile mtandao, tarakilishi, video, redio, simu, setelaiti, barua pepe, runinga, vipakatalishi, zote zinaweza kutumiwa kurahisisha mawasiliano darasani, kujenga kumbukumbu ya wanafunzi, kuwapa nafasi ya kutafiti mada tofauti, kufurahia kujifunza, kupata uhalisa wa yale wanayojifunza na hata kufanyia mazoezi teknolojia tofauti kwa maandalizi ya ulimwengu wa kazi. Pia idadi ya wanafunzi inaendelea kupanda ikilinganishwa na waalimu wanaotakiwa kushughulikia wanfunzi hawa. Kwa vile Kiswahili ni somo la lazima teknolojia hizi zingekumbatiwa ingekuwa rahisi sana mwalimu kufunza stadi kwa wanafunzi wengi wakati mmoja hata wakiwa katika maeneo tofauti. Teknolojia ibuka huzingatia fahiwa tofauti hasa za kusikiliza na kuona. Redio, epurekoda, runinga, simu za mkononi zinaweza kutumiwa kufunza stadi ya kusikiliza. Tepurekoda, kanda za video, runinga zinaweza kutumiwa kufunza stadi ya kuzungumza. Stadi ya kusoma inaweza kufunzwa kwa kutumia mtandao, vifaa vya kurekodi sauti, nayo stadi ya kuandika inaweza kufunzwa kwa kutumia simu za mkononi, runinga, mtandao au video. Wanafunzi wanaweza kupata ujumbe, ufafanuzi kwa kutafiti mtandaoni. Inatarajiwa kuwa waalimu na wanafunzi wa somo la Kiswahili watazingatia teknolojia ibuka kuelewa somo hili na kupata umilisi wa kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano.



**Maneno muhimu:** Maudhui, riwaya, tashtiti, umajazi, umuundo, wahusika.

**UTANGULIZI**

Maswala ya elimu yanatiliwa maanani sana na mataifa mengi duniani na hasa yale yanayoendelea likiwemo bara la Africa. Tangu kujinyakulia uhuru Kenya imejitahidi kuboresha mfumo wa elimu ili kuafiki matakwa yake. Lengo lake ni kuwa elimu bora itabadili uchumi na maisha ya watu wake. Kamau (2014) anasema juhudi hizi ni njia mojawapo ya kuboresha uchumi kama ilivyo katika mataifa yaliyoendelea. Ili kuafiki malengo ya elimu, mfumo wa elimu unajumlisha masomo tofauti kama lugha, sayansi, hisabati, sayansi kimu na mengine (KIE, 2002).

Kiswahili ni mojawapo ya masomo ya lazima katika shule za msingi na za upili nchini Kenya. Katiba inatambua Kiswahili kama lugha rasmi na pia lugha ya taifa (Republic of Kenya, 2010). Lugha hii inatumiwa katika mawasiliano na asilimia themanini ya wakenya (Odeo, 2003). Mfumo mpya wa elimu, Competency Based Curriculum (CBC), unatilia mkazo somo la Kiswahili. Mojawapo ya mbinu za kutathmini wanafunzi itakuwa ni uwezo wao kuwasiliana kupitia lugha na hasa Kiingereza na Kiswahili. Kwa hivyo ufunzaji wa somo la Kiswahili lazima uzidi kuboreshwa ili kuafiki malengo ya elimu.

Teknolojia za kisasa zimebadili pakubwa njia za mawasiliano na utendakazi kwa jumla. UNACTAD (2018) wanasema teknolojia hizi zinaweza kutumiwa kukabiliana na changamoto za kiuchumi, kijamii, na kimazingira. Tenolojia ibuka sas zinatumiwa katika sekta kama vile afya, biashara, usafiri, utawala, kilimo, viwanda, ufundi n ahata elimu. Wakati wa mkurupuko wa janga la korona, shule na vyuo, vilizingatia masom ya mtandaoni kupitia vifaa vya kisasa. Somo la Kiswahili pia lilifunzwa kupitia teknolojia hizi. Ilibidi walimu kuwa wabunifu ili kutumia teknolojia ibuka kuwafikia wanafunzi kwani vikao vya watu wengi vilikuwa vimepigwa marufuku.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

**Dhana ya Teknolojia**

Teknolojia ni elimu ya sayansi inayohusu uundaji na utumiaji wa mitambo. Mrikaria (2007) anafafanua teknolojia kama maendeleo ya kisayansi ambayo yanaweza kuonekana na hata kutumiwa. Anaendelea kusema kuwa teknolojia ibuka ni uvumbuzi na matumizi ya vifaa na mitambo ya kisasa katika mawasiliano na shughuli zingine nyingi za bianadamu. Robinson (2008) naye anafafanua teknolojia kama vifaa na maarifa yanayotumiwa katika uzalishaji wa vitu au huduma kwa manufaa ya binadamu. Teknolojia ibuka zimetumiwa kuboresha uhusiano kati ya watu, kurahisisha na kuboresha mawasiliano. Pia zimepanua ujuzi na kuhifadhi habari muhimu kwa binadamu.

Murray na Waller (2007) wanakiri kuwa matumizi ya teknolojia katika ufunzaji yanawezesha shughuli za elimu kufanyika mahali popote na wakati wowote. Manufaa ya teknolojia katika elimu yanaelekea kushawishi watafiti na hata washika dau katika sekta hii kupigia debe matumizi yake katika mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji (Johnson, 2007). Mrikaria (2007) anapendekeza matumizi ya teknolojia kama mtandao, tarakilishi, redio, video, simu, setelaiti, barua pepe, runinga, vipakatalishi; vitumiwe katika uhifadhi n ahata usambazaji wa Fasihi. Teknolojia hizi pia zinaweza kutumiwa katika ufunzaji wa somo la Kiswahili. Mtaala wa elimu unatilia mkazo matumizi ya nyenzo na mbinu tofauti katika ufunzaji ili kusisimua na kuwezesha wanafunzi kukumbuka waliyosoma (KIE, 2002).

**Teknolojia Ibuka katika Mchakato wa Ufunzaji na Ujifunzaji**

Matumizi ya teknolojia katika elimu imeshika kasi katika karne ya 21. Derek (2003) anasema kuwa teknolojia ibuka zinamwezesha kupata ujumbe kwa urahisi, kufanya utafiti mwingi, kupata na kuchuja habari kulingana na mada. Pia mwanafunzi anapata nafasi ya kulinganisha masomo ya darasani na hali halisi au hata ulimwengu wa kazi ambao atakumbana na baada ya shule. Ujuzi anaopata anapotumia teknolojia hizi unampa tajriba tosha atakayotumia anapojiajiri au kuajiriwa. Kwa mfano, mwanafunzi anajifunza kutafiti mtandaoni, kuwasiliana kupitia barua pepe, kurekodi habari n ahata kutafsiri habari zilizorekodiwa. Kulingana na Grabe and Grabe (2007) ujuzi wa kutumia tarakilishi ni lazima kabla mtu kuajiriwa kazi katika ulimengu wa sasa.

Mabadiliko katika elimu hulenga kuboresha na kutoa elimu sawa kwa wananchi wote, (KIE, 2002). Hali hii huchangia ukuaji wa uchumi wa nchi. Tafiti zilizofanywa zinaonyesha kuwa teknolojia ibuka zikitumiwa katika mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji humfaidi san mwalimu na mwanafunzi. Wims and

Crawler (2007) walipata kuwa teknolojia hizi huhifadhi ujumbe ili utumiwe baadaye, au huweza kufidia upungufu wa walimu kama hali ilivyo sasa. Mwalimu mmoja anaweza kuwafundisha wanafunzi wengi hata wakiwa katika maeneo tofauti.

Juhudi za serikali kusambaza umeme na nyenzo za kisasa mashuleni inaonyesha namna ambavyo uongozi wa taifa hili unatilia mkazo maswala ya elimu. Wanaelewa kuwa elimu ndio msingi wa maendeleokatika taifa lolote. Kutokana na juhudi za serikali na washika dau wengine, utafiti huu ulidhamiria kuchunguza namna juhudi hizi zinachangia ufunzaji wa somo la Kiswahili. Ikumbukwe kuwa Kiswahili ni somo shuleni na pia lugha muhimu sana katika mawasiliano.

**Nadharia ya Utafiti**

Utafiti huu ulizingatia nadharia ya Piaget (1971) inayosema kuwa akili ya mtoto hukua kulingana na mtagusano wake na mazingira. Ni mazingira ambayo humfikirisha mtoto, kunoa ubongo wake na kumsaidia kuwa mbunifu. Ubunifu huu unamwandaa kukabiliana na maisha yake ya baadaye. Piget katika nadharia yake anapendekeza kuwa mwanafunzi aandaliwe mazingira yanayomwezesha kutagusana na mada tofauti zinazofunwa kwa kutumia nyenzo tofauti. Hali hii itamwzesha kuona hali halisi, kufikiria na kujenga taswira yay ale anayoona na kusikia. Mwishowe taswira hizi hunata akilini mwake.

Young (1993) anakubaliana na maoni ya Piaget anaposema katika utafiti wake kuwa ujifunzaji hutokea wakati mwanafunzi anatapogusana na nyenzo na mazingira yanayolingana na mada inayofunzwa. Kwa kurejelea utafiti huu, mwalimu na mwanafunzi wa somo la Kiswahili wanahitaji kuzingatia teknolojia ibuka katika kuandaa mazingira faafu ya ufunzaji wa mada tofauti kama lugha, fasihi, ushairi au hata uandishi wa insha. Mwalimu anaweza kurekodi Makala katika video au redio na kuyatumia kufunza mada katika fasihi, insha au kipengele cha isimu jamii. Pia mwalimu anaweza kuhifadhi rekodi ya mawsilisho ya fasihi simulizi katika video na kuwaonyesha wanafunzi anapofundisha vipengele kama nyimbo, densi, mazungumzo au maigizo.

Kwa kutumia simu tamba wanafunzi wanaweza kutafiti mada tofauti kwa mtandao na hivyo basi kujiongezea maarifa. Shule nyingi zina tarakilishi ambazo wanafunzi wanaweza kutumia kujipa maarifa ya utafiti au kuandika. Maarifa haya yatawafaa hata baada ya shule wanapoingia katika ulimwengu wa kazi. Itakuwa bora kama ufundishaji wa Kiswahili utalenga uamilifu wake katika shughuli za kila siku na sio tu kukariri kaida za lugha pengine kwa lengo la kupita mtihani.

**Uhakiki wa Maandishi**

Kila uchao ulimwengu unazidi kubadilika kwa uvumbuzi wa sayansi na teknolojia. Kila shughuli sasa inafanyika kwa kuzingatia teknolojia za kisasa. Katika muktadha wa elimu teknolojia hizi hazijasazwa. Miruka (1999) anarejelea methali ya Wachina kuwa;

“Nikisikiacho, nakisahau,
Nikionacho, nakikumbuka,
Nikifanyacho, nakikumbuka zaidi. ”

Methali hii inatilia mkazo matumizi ya nyenzo ambazo zinampa mwanafunzi nafasi ya kutenda zaidi katika mchakato wa kujifunza. Teknolojia za kiasasa kama tarakilishi, barua pepe, simu za mkononi, zote zinahitaji mwanafunzi mwenyewe kutekeleza kwa hivyo atakumbuka zaidi. Katika somo la Kiswahili mwanafunzi anaweza kurekodi Makala na kuyatazama au kuyasikiliza mwenyewe. Pia anaweza kufanya utafiti kuhusu mada tofauti kwa kutumia mtandao.

Badiribu (1985) alitafiti mbinu za kufundishia Ushairi katika somo la Kiswahili. Alipata kuwa walimu hutumia picha na maelezo ili kurahisisha somo hili ambalo wanafunzi wengi hulichukulia kuwa gumu. Picha hizi n ahata maelezo yanaweza kupatikana kupitia teknolojia ibuka kama utafiti huu unavyopendekeza. Kamera za kidijitali, kanda za video na hata mtandaoni kuna picha ambazo zikitazamwa zinaleta uhalisia na kumfikirisha mwanafunzi; hupunguza maelezo maelezo marefu ambayo husahaulika papo hapo. Mbuthia (1996) anakubaliana na maoni haya anaposema kuwa, ili kuondoa ugumu wa kufikirika katika somo la Ushairi, walimu wawe wabunifu na kutumia teknolojia za kisasa wanapofunza Ushairi. Wanafunzi wa leo wanapendelea teknolojia hizi kwa hivyo zikitumiwa kufundishia Ushairi na hata vipengele vingine, somo la

Kiswahili litawavutia Zaidi. Silabasi ya Kiswahili (KIE, 2002) pia inatilia mkazo matumizi ya nyenzo tofauti katika ufundishaji ili kumakinisha wanafunzi.

Mwandishi Liyong (1972) anawakumbusha wanafunzi kutilia mkazo tamaduni zao walizofunzwa na akina babu, nyanya, shangazi, wajomba, baba na mama. Ikiwezekana walete mafunzo haya katika madarasa ya leo ili kukuza utamaduni. P'Bitek (1974) naye anasema kuwa watafiti waende nyanjani kuhudhuria na hata kushiriki katika mawasilisho ya Fasihi Simulizi moja kwa moja. Ngure (2004) anakubaliana na maoni haya anaposema kuwa Fasihi Simulizi inavutia zaidi mtu anaposhiriki moja kwa moja. Kulingana na utafiti wa sasa wanafunzi wanaweza kuhusishwa zaidi katika mawasilisho kwa kutazama makala yaliyorekodiwa kwenye video, filamu, televisheni, mtandao na pia kusikiliza redio. Inawezekana wanafunzi kuona na kusikia Makala kuhusu tamaduni tofauti katika maeneo tofauti ya ulimwengu.

Syambo na Mazrui (1996) wanasema kuwa awali Fasihi Simulizi iliwasilishwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo na nyenzo za kitamaduni kama ngoma, maleba. Leo Fasihi hii imehifadhiwa na inaweza kupatikana kupitia teknolojia kama redio, televisheni, tarakilishi, video na mawsiliano ya setelaiti. Nyenzo hizi ni kivutio kwa wanafunzi wa leo. Mogambi (2004) anawahimiza walimu kuzingatia mbinu na nyenzo za kisasa kufundishia somo la Kiswahili. Hii ni kwa sababu kizazi cha sasa kina maarifa na ujuzi mwingi kutokana na mtandao. Wanajua kutumia hata wengine kuliko walimu wao. Ikiwa walimu watatumia njia zinazorahisisha maelezo na kuwavutia wanafunzi mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji utazaa matunda. Ndipo utafiti huu unapendekeza matumizi ya teknolojia za kisasa.

Utafiti wa Wamitila (2005) unapendekeza wanafunzi wakusanye data kutoka tamaduni zao na kuitmia katika somo la Fasihi Simulizi. Kwa mfano wanaweza kuchukua picha wakitumia simu za mkononi au kamera za kidijitali, kurekodi fanani au wasilisho katika video. Nyenzo hizi zinahifadhi ujumbe ili utumiwe unapohitajika. Makala yaliyorekodiwa yanaweza kutumiwa wenzao katika maeneo tofauti. Kubadilishana makala hivi kunaweza kuwatia wanafunzi motisha ili kushirikiana katika ujifunzaji wao.

Kulingana na Suter na Busienei (2012) utafiti wao unaonyesha kuwa shule nyingi zina vitabu tu hivyo basi walimu wengi huzingatia tu hivo vibu na maelezo katika ufunzaji wa somo la Kiswahili. Hali hii ilichangia ukavu na matokeo duni katika somo hili katika Wilaya ya Marakwet. Inelekea kuwa wanafunzi walisahau maelezo ya mwalimu haraka na walikosa mvuto katika ujifunzaji. Kama walimu wangekuwa wabunifu na kutumia teknolojia ibuka zinazowavutia wanafunzi hali ingekuwa tofauti. Na ndiyo sababu utafiti wa sasa unapendekeza matumizi ya teknolojia za kisasa.
Tafiti nyingi zinaonyesha kuwa walimu wakiboresha mazingira ya darasa matokeo ya wanafunzi yataimarika (Oduro, 2008). Walimu wanaweza kuboresha mazingira ya darasa kwa kutumia teknolojia za kiasasa.

**MATOKEO YA UTAFITI**

**Nyenzo za Kufunzia Shuleni**

Utafiti huu ulipata kuwa shule nyingi zina walimu wa Kiswahili waliohitimu. Hata hivyo, walimu hawa wana kazi nyingi kwani wanafunza somo la pili na pia idadi ya wanafunzi darasani ni kubwa. Walikiri kuwa wan nyenzo tofauti ambazo wanatumia kufunza somo la Kiswahili. Walitoa mifano ya nyenzo kama redio, televisheni, picha, ramani, chati, fanani, sehemu za mawasilisho, filamu, video, modeli, magazeti, vitabu, vifaa halisi, ubao na zingine nyingi. Walimu pia huandaa ziara za nyanjani na kutumia uigizaji wanapofunza baadhi ya vipengele. Maoni ya walimu hawa yanafikiana na utafiti wa Wasiche (2009) kuwa kuna nyenzo tofauti shuleni na zinatumiwa kufunza somo la Kiswahili.

Kuhusu teknolojia ibuka mtafiti alipata kuwa katika shule nyingi kuna nyenzo za kisasa kama vile redio, televisheni, tarakilishi, projekta, mtandao, simu za mkononi, setelaiti, mikanda ya video, diski, filamu na kamera za kidijitali. Hii inamaanisha kuwa shule zimejitahidi kujipayia teknolojia za kisasa ili zitumiwe katika mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji. Serikali ikishirikiana na mashirika kama Safaricom, Nokia, Airtel na Samsung inatoa huduma za mtandao kwa shule nyingi. Mashirika kama e-limu, ed-tech tablet initiative, School-Net, yametoa tarakilishi kwa shule ili ziyumiwe

katika ufunzaji na utafiti. Hazina za maendeleo bungeni (NG-CDF), wazazi, na washikadau wengine pia wamechangia kununua au kutoa msaada wa nyenzo za kiasasa katika baadhi ya shule. Mtafiti alipotembelea shule alithibitisha kuweko kwa teknolojia za kisasa ambazo zimetajwa.

**Matumizi ya Teknolojia za Kisasa katika Mchakato wa Ufunzaji na Ujifunzaji**

Mtafiti alipata kuwa walimu wengi walifahamu nafasi ya teknolojia ibuka katika ufundishaji. Wengi walikiri kuwa wametagusana na teknolojia ibuka hata nje ya darasa. Kila mwalimu alikiri kuwa na simu ya mkononi na kuelewa namna ya kutumia mtandao kwa shughuli tofauti.

Tarakilishi zilikuwepo katika shule zote. Kando na kutumiwa katika shughuli za usimamizi wa shule, baadhi ya walimu walizitumia katika ufunzaji. Walizitumia walisema kuwa wliziunganisha kwenye projekta ili kuonyesha picha au video zikiambatana na sauti kwa manufaa ya wanafunzi. Walitumia njia hii kufunza vipengele vya Fasihi ili kuleta uhai na uhalisia darasani. Wanfunzi pia walipewa nafasi ya kutumia tarakilishi na mtandao kufanya utafiti wa mada tofauti, kujifunza kuchora na kuandika wakitumia tarakilishi. Mazoezi kama haya ni bora kwa wanafunzi ikichukuliwa kuwa karne ya 21 inahitaji ujuzi wa tarakilishi kutekeleza shughuli mbalimbali.

Simu za mkononi zilitumiwa na walimu katika mawasiliano yao ya kibinafsi mara nyingi. Baadhi ya walimu walitumia simu hizi kutafiti mada, kuonyesha michoro, picha na video wakati wa kufunza. Walimu walikubali kuwa simu zinaweza kutumiwa pamoja na projekta picha na maandishi makubwa darasani. Ili kufunza matamshi katika somo la Kiswahili walimu walirekodi wanafunzi wakitamka sauti na kuwachezea ili waelewe matamshi yao. Vile vile uigizaji kama katika kipengele cha Isimu Jamii kingefunzwa kwa njia hii. Simu pia zilitumiwa kupokezana ujumbe kati ya walimu kuhusu taaluma na tajriba zao katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Wengi wao wilikiri kuwa wamo katika makundi kama vile ya Watsupp, wanatumia Twitter, YouTube kupashana ujumbe. Hii inachangia kuboresha taaluma yao.

Mtandao pia ulikuwepo katika shule za utafiti. Shule nyingi zilipata huduma za mtandao kutoka kwa mashirika kama Safaricom, Airtel na Telekom. Shule chache zilikuwa na huduma za setelaiti. Mtandao ulitumiwa katika shughuli za utafiti wa za kufunzwa. Wanafunzi waliruhusiwa kutumia huduma za mtandao ili kufanya utafiti wa kielimu. Shughuli hii ilifanywa katika maktaba au maabara ya Tarakilishi. Walimu na wanafunzi waliohojiwa walisema walifurahia matumizi ya intaneti katika utafiti kwani ilipanua ujuzi na maarifa yao. Waliweza kuwasiliana kupitia barua pepe ambao ni mtindo wa kisasa wa kutuma na kupokea barua. Walimu wachache walikiri kutumia mbinu ya masomo ya mtandaoni, 'e-learning', wakati wa mkurupuko wa janga la Korona wanafunzi wote walipokuwa nyumbani.

Mtafiti pia alipata kuwa shule chache zilikuwa na kamera za kidijitali. Walimu walikiri kuwa ingawa kamera hizi zilikuwepo hawakuzitumia katika ufunzaji wa somo la Kiswahili. Kamera ziliwekwa tu katika Afisi na kutumika tu katika hafla rasmi za shule. Badala yake walimu walitumia simu za za mkononi kuchukua picha za kutumia katika ufunzaji. Ingekua bora kama kamera hizi zingetumiwa kwa sababu hutoa picha nzuri na pia wanafunzi wangejifunza maarifa ya kutumia kamera hizi kwa manufaa yao ya baadaye.

Shule zote za utafiti zilikuwa na runinga. Kifaa hiki kilihifadhiwa katika chumba cha maankuli ili wanafunzi watazame taarifa wakati wa chakula au wakati wao wa burudani. Runinga zingine zilikuwa katika vyumba maalum vya walimu. Walimu hawakutumia runinga kufunza somo la Kiswahili darasani lakini wanafunzi walipewa fursa ya kutazama vipindi muhimu kuhusiana na somo la Kiswahili kama vile taarifa za habari, uchambuzi wa lugha, kazi za fasihi, habari za michezo na vipindi vingine faafu. Inaonekana mjio wa runinga na simu za mkononi ulinyima nafasi redio kama nyenzo katika ufunzaji, Shule hazikuwa na redio ingawa mtafiti anapendekeza matumizi ya nyenzo hii katika muktadha wa ufunzaji ili kuandaa wanafunzi kwa taaluma ya mawasiliano.

Kanda za video pia zilikuwepo na zilitumiwa katika ufunzaji wa somo la Kiswahili. Baadhi ya kazi za Fasihi zilizohifadhiwa katika kanda za video zilionyeshwa wanafunzi kupitia runinga na tarakilishi. Picha na

maelezo ya fanani kupitia kanda za video yalileta hali halisi darasani na kunata akilini mwa wanfunzi kulingana na walimu waliohojiwa.

**Umuhimu wa Teknolojia Ibuka katika Ufunzaji wa somo la Kiswahili**

Kutokana na utafiti huu, walimu walikiri kuwa kuna manufaa chungu nzima ya kutumia teknolojia za kiasasa katika ufunzaji wa somo la Kiswahili. Kulingana na utafiti wa Mrikaria (2007) uliolenga Fasihi Simulizi, teknolojia za kisasa zinaweza kutumiwa kuhifadhi vipengele vya Fasihi Simulizi. Makala yaliyohifadhiwa ni ya hali ya juu na yanaweza kuwafikia wanafunzi wa wengi kwenye maeneo tofauti. Anataja nyenzo kama vile video, runinga, tarakilishi, tovuti, setelaiti na simu za mkononi kama mifano ya teknolojia za kuhifadhi na kuonyesha makala. Anaendelea kusema kuwa teknolojia hizi zinaweza kuunganisha fanani na wanafunzi darasani;pia kufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Utafiti huu unakubaliana na maoni haya na kuongezea kuwa vipengele vingine vya somo la Kiswahili kama Riwaya, Tamthilia, Ushairi, Kusoma na Kuandika vinaweza kufunzwa kwa kutumia njia hizi.

Mawasiliano kupitia mtandao na setelaiti yanaweza kuwafikia wanafunzi moja kwa moja au kupitia Makala yaliyorekodiwa. Wanafunzi wanaweza kutazama runinga, video, au kusikiliza hali halisi ya matamshi yao, au matumizi ya lugha katika maeneo tofauti, (Rebecca & Marshal, 2014). Maswala ibuka ni muhimu katika ufunzaji wa lugha. Humwezesha mwanafunzi kutagusana na hali halisi inayomzunguka, kufikiri na kukata kauli yeye mwenyewe binafsi. Maswala haya yanapatikana katika mtandao na vyombo vya habari kama magazeti, redio, runinga, na simu za mkononi. Robertson (2000) aligundua katika utafiti wake kuwa teknolojia za kiasas zinawapa wanafunzi nafasi ya kutafiti mambo mengi, mengine ya kisasa kabisa. Kwa mfano, janga la 'Korona' limefafanuliwa Zaidi kupitia mtandao, redio, runinga na simu za mkononi. Wanafunzi wanaweza kutumia ujumbe walioupata kutokana na utafiti kutunga insha, kushiriki katika mijadala, kuigiza hali halisi n ahata kufanya uamuzi utakaokuwa muhimu katika maisha yao ya sasa na hata baadaye.

Robertson (2008) akitafiti matumizi ya mtandao katika ufunzaji alipata kuwa teknolojia ibuka zinaweza kufikisha ujumbe kwa wanafunzi wengi hata wakiwa katika maeneo tofauti kijiografia. Kwa kurejelea utafiti huu, mwalimu wa somo la Kiswahili anaweza kufuna kupitia mtandao ikiwa wanafunzi wake wana simu na wanaweza kupata intaneti. Si lazima wakutane ana kwa ana. Barua pepe zinaweza kuwa njia haraka na rahisi kutumika katika mawsiliano. . Pia wanaweza kuandaa mjadala mtandaoni na kuchangiana maoni kutoka kokote waliko. Wanaweza kutumia simu zao kuwasiliana kuhusu mada za kielimu kupatia kurasa kama 'Facebook, twitter, watsuup na Youtube'. Vijana watafurahia mbinu kama hizi katika ujifunzaji wao.

Kulingana na Suter na Busienei (2007) kwenye utafiti wao uliohusu nyenzo na mbinu za kufundishia Fasihi Simulizi, walipata kuwa wanafunzi wanaweza kutazama maigizo ya Tamthilia, Riwaya, na Mashairi yaliyorekodiwa. Awali makundi ya Sanaa yalitembelea shule za upili wakiigiza vitabu vya Fasihi. Hali si hivyo tena leo. Ni Makala yaliyorekodiwa katika video ambayo huonyeshwa wanafunzi ili kuchangia ufundishaji wa darasani.

Hali halisi inaweza kuwafikia wanafunzi wakachora taswira na kukumbuka mambo kupitia teknolojia za kisasa. Kwa kutazama picha kwenye simu au tarakilishi mwanafunzi anaweza kuona pwani ya Kenya ambayo ni Kitovu cha lugha ya Kiswahili. Video za maisha ya Waswahili zinaweza onyeshwa ili hali halisi ya maisha ya Waswahili iwafikie wanafunzi hata bila wao kuzuru sehemu za pwani. Maonyesho kama haya yanaweza kusisimua fikra na kujenga ubunifu wa wanafunzi.

Amali na tamaduni za kijamii awali zilipitishwa kwa njia ya mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kulingana na Wetende (2016) wazee wenye busara hizi wanaendelea kupungua kutokana na umri wao. Kupitia teknolojia za kisasa kama video na tepurekoda masimulizi ya wazee hawa yanaweza kurekodiwa na kuhifadhiwa kwa matumizi ya baadaye. Mwalimu anaweza kurekodi masimulizi ya hadithi za kale, maigizo, nyimbo na densi, au tanzu fupi na kuwaonyesha wanafunzi anapofunza kipengele husika. Hifadhi hii pia ni muhimu kwa taifa kurithisha mila na tamaduni kwa vizazi vichanga.

Licha ya manufaa mengi ya teknolojia ibuka katika ufunzaji na hasa somo la Kiswahili, mtafiti alipata

kuwa qalimu wengi hawakutumia teknolojia hizi kataka ufunzaji. Walitegemea tu vitabu ambavyo serikali imetoa kwa wingi katika shule hasa zile za umma. Pia kazi nyingi ndani ya muda mchache ilijitokeza kama sababu ya walimu wengi kutovalia njuga matumizi ya teknolojia za kisasa. Baadhi ya walimu walilalamikia kutokuwa na ujuzi wa kutumia teknolojia hizi kwa hivyo waliziepuka.

## HITIMISHO NA PENDEKEZO

**Hitimisho:** Teknolojia za kisasa ni nguzo muhimu sana katika maendeleo duniani kote. Katika muktadha wa elimu teknilojia hizi zina manufaa chungu nzima. Utafiti huu ulilenga tu kuchunguza teknolojia za kisasa na matumizi yake katika ufunzaji wa somo la Kiswahili. Ingawa teknolojia hizi zinapatikana kwa urahisi shuleni na walimu walielewa umuhimu wake bado hawakuzitumia katika shughuli za kufunza. Wengine kwa kutokuwa na ujuzi walikwepa kutumia teknolojia hizi. Mtafiti anapendekeza utafiti mwingine kufanywa ili kuelewa kwa nini walimu hawakushabikia kutumia teknolojia ibuka katika ufunzaji na hasa somo la Kiswahili ilhali wanaelewa umuhimu wake.

**Pendekezo:** Inatarajiwa kuwa matokeo ya utafiti huu yatachangia uundaji wa sera kuhusu matumizi ya teknolojia za kisasa kufunza somo la Kiswahili na hata masomo mengine. Dunia ya sasa ni ya teknolojia na wanafunzi wetu wanapotagusana nazo mapema inawaandaa kwa ulimwengu wao wa kazi na maisha yao ya baadaye. Hao ndio watakaokuwa watafiti na wabunifu wa teknolojia zingine bora Zaidi kuliko zilizoko sasa.

## MAREJELEO


Badiribu, M. D. (1995). *Kielelezo cha Kufundisha Mashairi Yetu.* M. ED Thesis. Kenyatta University. (Unpublished).

Derek, S. (2003). ICT Definitions. https://derekstockley.com.au/elearninglet.html

Grabe, M., & Grabe, C. (2007). *Integrating Technology for Meaningful Learning*. (5th ED). Houghton Mufflin.

Johnson, H. M. (2007). *Dialogue and Construction of Knowledge. Exploring Students'Perception of Their Learning*. Eurodl.org

Kamau, L. M. (2014). *Technology Adoption in Secondary Mathematics Teaching in Kenya*.

KIE. (2002). *Mtaala wa Kiswahili nchini Kenya*. Nairi.

Laaria, M. (2013). Leadership Challenges in the Implementation of ICT in Public Secondary Schools in Kenya. *Journal of Education and Learning*.

Liyong, T. (1972). *Popular Culture of East Africa*: Oral Literature. East African Educational Publishers.

Mbuthia, F. (1996). *A Comparative Study of the Effects of Two Instructional Approaches on Student Performance in Kiswahili Poetry in Selected Schools in Eldoret Municipality.* Unpublished M. Phil Thesis. Moi University.

Miruka, O. (1999). *Oral Literature for Schools*. East African Educational Publishers.

Mogambi, H. (2004). *Mwelekeo wa Lugha. Walimu Waambiwa Wafunze kwa Njia Rahisi Kueleweka.* Katika Taifa Leo, 26/2 2002. Nation Media Group.

Mrikaria, S. E. (2007). Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya. *Swahili Forum*, 14, 197 – 206.

Murray, K., & Waller, R. (2007). *Social Networking goes abroad. Education Abroad*, 16(3), 56-59.

Ngure, A. (2004). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Phoenix Publishers.

Odeo, I. (2003). *Oral Questioning in Pedagogy of Kiswahili Grammer. A study of Teachers' Practices in Bungoma District*. Unpublished DPhil Thesis. Moi University.

Oduro, P. (2008). *A Survey of Instructional Practices of Kiswahili Teaching in Upper Primary Schools.* Unpublished M. ED Thesis, University of Nairobi.

P'Bitek, O. (1974). *Horn of my Love*. Heinemann Educational Publishers.

Passey, D. (2013). *Inclusive Technology Enhanced Learning. Overcoming Cognitive, Physical, Emotional and Geographic Challenges*. Routledge.

Piaget, J. (1971). *The Theory of Stages in Cognitive Development.* Routledge.

Rebecca, W., & Marshal, S. (2014). *A New Face of Education. Bringing Technology into the Classroom in the Developing World.* Brookings.

Robertson, B. (2000). *Integrating Technology into the Classroom*. http:/www.infotody. com/mmschools/mar 00/Robertson, HTM
Robinson, B. (2008). *Using Distance Education and ICT to Improve Access, Equity and Equality in Rural Areas*. http:/www. irodl.org.index.php.html
Suter, E., & Busienei, A. (2012). Materials and Instructional Approaches used by Secondary School Teachers of Kiswahili Oral Literature in Marakwet District, Kenya. *JETERAPS, 4*(3), 566-574.
Syambo, B. K., & Mazrui, A. M. (1996). *Uchambuzi wa Fasihi*. East African Educational Publishers.
UNACTAD. (2018). Ripoti ya Umoja wa Mataifa ya Biashara na Uchumi na Maendeleo. *Malengo ya Maendeleo Endelevu.*
Wabuyela, L. C. (2003). *Understanding Teachers and Administrators Perceptions and Experiences towards Computer Use in Kenya. A Case of Two Schools.* Ohio University.
Wamitila, K. W. (2005). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Focus Books.
Wasiche, F. A. (2009). *A Survey of the Use of Instructional Media in Teaching Oral Literature in Kiswahili in Secondary Schools in Bungoma South District, Kenya*. Unpublished M. Phil Thesis, Moi University.
Wetende, C. M. (2016). Utilization of Educational Media in Teaching and Learning Oral Literature in Butere Sub-County Secondary Schools. *IJSR, 5*(11).
Wims, P., & Lawler, M. (2007). *Investigating ICTs in Educational Institutions in Developing Countries. An Evaluation of their Impact in Kenya*. http://jedict. uwi.ed/printarticle.html
Young, S. (1993). *Learning Theories and Instructional Design*. Prentice Hall Inc.